



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



KUMB: PPR/2023 - 3/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 MACHI 2023**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Machi 2023**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Kwa Machi 2023, bei za rejareja za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** yamepandaa kwa shilingi 149/Lita, shilingi 25/lita na shilingi 37/lita, mtawalia, ikilinganishwa na toleo la tarehe 1 Februari 2023.
- (b) **Kwa Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara)**, bei za rejareja za Machi 2023 kwa mafuta ya petroli na dizeli yanapungua kwa shilingi 64/Lita na shilingi 209/lita, mtawalia, ikilinganishwa na toleo la tarehe 1 Februari 2023. *Kutokana na kuisha kwa mafuta ya taa kwenye matanki ya kuhifadhia yaliyopo Tanga, waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*
- (c) **Kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)**, bei za rejareja za Machi 2023 kwa mafuta ya petroli zinaongezeka kwa shilingi 138/lita wakati bei ya mafuta ya dizeli zinapungua kwa shilingi 68/lita. *Kwa kuwa hakuna matanki ya kuhifadhia mafuta ya taa katika bandari ya Mtwara, waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kusini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*

Bei za miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 1**.

Tofauti ya bei kutoka sehemu moja kwenda nyingine inatokana na tofauti ya bandari mafuta yanapochukuliwa na gharama ya usafirishaji.

Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) na thamani ya shilingi ukilinganisha na dola ya kimarekani.

Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

- (a) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (*Price cap*) au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (*Floor Price*) kama ilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 la tarehe 28 Januari 2022.**
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (e) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la

kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

- (f) **Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 1. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**
- (g) **Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 2 isipokuwa kwa wateja wenye msamaha wa kodi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,968	3,130	3,098
Arusha	2,971	3,188	3,182
Arumeru (Usa River)	2,971	3,188	3,182
Karatu	2,989	3,206	3,200
Longido	2,982	3,199	3,193
Monduli	2,977	3,193	3,188
Monduli-Makuyuni	2,981	3,198	3,192
Ngorongoro (Loliondo)	3,056	3,272	3,274
Coast (Kibaha)	2,972	3,134	3,103
Bagamoyo	2,979	3,141	3,109
Bagamoyo (Miono)	3,009	3,172	3,140
Bagamoyo (Mbwewe)	2,990	3,153	3,121
Chalinze Junction	2,982	3,144	3,112
Chalinze Township (Msata)	2,986	3,148	3,116
Kibiti	2,988	3,150	3,118
Kisarawe	2,975	3,137	3,105
Mkuranga	2,977	3,140	3,108
Rufiji	2,995	3,157	3,126
Dodoma	3,026	3,189	3,157
Bahi	3,034	3,196	3,164
Chamwino	3,022	3,184	3,152

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Chemba	3,053	3,215	3,183
Kondoa	3,059	3,221	3,190
Kongwa	3,024	3,186	3,154
Mpwapwa	3,028	3,190	3,158
Mpwapwa (Chipogoro)	3,040	3,202	3,170
Mtera (Makatopora)	3,045	3,208	3,176
Mvumi	3,033	3,195	3,163
Geita	3,133	3,295	3,263
Bukombe	3,122	3,284	3,252
Chato	3,154	3,316	3,285
Mbogwe	3,171	3,333	3,302
Nyang'hwale	3,148	3,310	3,278
Iringa	3,032	3,194	3,162
Ismani	3,037	3,199	3,167
Kilolo	3,036	3,198	3,167
Mufindi (Mafinga)	3,042	3,204	3,172
Mufindi (Igowole)	3,050	3,213	3,181
Kagera (Bukoba)	3,183	3,345	3,314
Biharamulo	3,157	3,320	3,288
Karagwe (Kayanga)	3,200	3,362	3,330
Kyerwa (Ruberwa)	3,205	3,368	3,336
Muleba	3,183	3,345	3,314
Ngara	3,171	3,333	3,301
Misenyi	3,192	3,354	3,322
Katavi (Mpanda)	3,125	3,288	3,256
Mlele (Inyonga)	3,107	3,269	3,237
Mpimbwe (Majimoto)	3,145	3,307	3,275
Tanganyika (Ikola)	3,143	3,305	3,274
Kigoma	3,130	3,292	3,260
Uvinza (Lugufu)	3,120	3,282	3,251
Muyobozi Village (Uvinza)	3,129	3,291	3,259
Ilagala Village (Uvinza)	3,131	3,293	3,261
Buhigwe	3,129	3,291	3,259
Kakonko	3,131	3,293	3,261
Kasulu	3,139	3,301	3,270
Kibondo	3,137	3,299	3,267
Kilimanjaro (Moshi)	2,961	3,177	3,172
Hai (Bomang'ombe)	2,964	3,180	3,175
Mwanga	2,954	3,170	3,165
Rombo (Mkuu)	2,978	3,194	3,193
Same	2,947	3,163	3,158
Siha (Sanya Juu)	2,967	3,184	3,178
Lindi	3,027	3,189	3,157
Lindi-Mtama	3,031	3,194	3,175
Kilwa Masoko	3,050	3,213	3,132
Liwale	3,062	3,225	3,178
Nachingwea	3,047	3,209	3,186

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Ruangwa	3,053	3,216	3,188
Manyara (Babati)	3,005	3,222	3,220
Hanang (Katesh)	3,016	3,232	3,231
Kiteto (Kibaya)	3,021	3,237	3,231
Mbulu	3,018	3,234	3,233
Simanjiro (Orkasumet)	3,037	3,254	3,252
Mara (Musoma)	3,133	3,296	3,264
Musoma Vijijini (Busekela)	3,146	3,308	3,277
Rorya (Ingirijuu)	3,140	3,303	3,271
Rorya (Shirati)	3,148	3,310	3,279
Bunda	3,125	3,287	3,255
Bunda (Kisorya)	3,137	3,299	3,268
Butiama	3,131	3,293	3,261
Serengeti (Mugumu)	3,142	3,304	3,272
Tarime	3,142	3,304	3,272
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	3,148	3,310	3,278
Mbeya	3,075	3,237	3,205
Chunya	3,084	3,247	3,215
Chunya (Makongolosi)	3,090	3,252	3,220
Chunya (Lupa Tingatinga)	3,091	3,254	3,222
Kyela	3,091	3,253	3,221
Mbarali (Rujewa)	3,059	3,221	3,189
Rujewa (Madibira)	3,072	3,234	3,203
Rujewa (Kapunga)	3,069	3,231	3,199
Rungwe (Tukuyu)	3,084	3,246	3,214
Morogoro	2,993	3,155	3,123
Mikumi	3,008	3,170	3,139
Kilombero (Ifakara)	3,030	3,193	3,161
Kilombero (Mlimba)	3,053	3,215	3,183
Kilombero (Mngeta)	3,042	3,204	3,172
Ulanga (Mahenge)	3,041	3,203	3,172
Malinyi	3,051	3,214	3,182
Kilosa	3,011	3,173	3,141
Gairo	3,011	3,173	3,141
Mvomero (Wami Sokoine)	3,003	3,165	3,133
Mvomero (Sanga Sanga)	2,993	3,155	3,123
Turian	3,018	3,180	3,148
Mtwara	3,013	3,176	3,170
Nanyumbu (Mangaka)	3,050	3,212	3,219
Masasi	3,030	3,192	3,196
Newala	3,035	3,197	3,203
Tandahimba	3,028	3,190	3,196
Nanyamba	3,028	3,190	3,196
Mwanza	3,118	3,280	3,248
Kwimba	3,136	3,298	3,266
Magu	3,126	3,288	3,256
Misungwi	3,112	3,274	3,243

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Sengerema	3,150	3,312	3,281
Ukerewe	3,177	3,340	3,308
Njombe	3,060	3,222	3,191
Njombe (Kidegembye)	3,081	3,243	3,211
Ludewa	3,098	3,260	3,228
Makambako	3,052	3,215	3,183
Makete	3,091	3,253	3,221
Wanging'ombe (Igwachanya)	3,058	3,220	3,188
Rukwa (Sumbawanga)	3,141	3,303	3,271
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	3,141	3,303	3,271
Kalambo (Matai)	3,148	3,310	3,278
Nkasi (Namanyeje)	3,154	3,316	3,285
Nkasi (Kirando)	3,164	3,326	3,294
Ruvuma (Songea)	3,099	3,261	3,221
Mbinga	3,112	3,274	3,234
Namtumbo	3,090	3,252	3,227
Nyasa (Mbamba Bay)	3,137	3,299	3,244
Tunduru	3,064	3,227	3,201
Shinyanga	3,097	3,259	3,227
Kahama	3,101	3,263	3,231
Kishapu	3,105	3,267	3,235
Ushetu (Nyamilangano)	3,113	3,275	3,243
Ushetu (Kangeme Village)	3,119	3,281	3,249
Salawe	3,110	3,273	3,241
Simiyu (Bariadi)	3,115	3,277	3,245
Busega (Nyashimo)	3,127	3,289	3,257
Itilima (Lagangabilili)	3,115	3,277	3,245
Maswa	3,108	3,271	3,239
Meatu (Mwanhuzi)	3,119	3,282	3,250
Singida	3,058	3,221	3,189
Iramba	3,070	3,233	3,201
Manyoni	3,043	3,205	3,173
Itigi (Mitundu)	3,058	3,221	3,189
Ikungi	3,054	3,216	3,184
Mkalama (Nduguti)	3,083	3,245	3,213
Songwe (Vwawa)	3,084	3,246	3,214
Songwe (Mkwajuni)	3,091	3,253	3,221
Ileje	3,088	3,250	3,218
Momba (Chitete)	3,093	3,255	3,224
Tunduma	3,088	3,250	3,219
Tabora	3,076	3,238	3,206
Igunga	3,076	3,238	3,206
Kaliua	3,089	3,251	3,219
Ulyankulu	3,086	3,248	3,217
Nzega	3,086	3,248	3,217
Sikonge	3,085	3,247	3,215
Urambo	3,086	3,248	3,216

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Uyui	3,082	3,244	3,213
Mpyagula	3,107	3,270	3,238
Tanga	2,915	3,131	3,144
Handeni	2,935	3,151	3,124
Kilindi	2,950	3,166	3,158
Korogwe	2,927	3,143	3,137
Lushoto	2,936	3,152	3,147
Mkinga (Maramba)	2,922	3,138	3,158
Muheza	2,919	3,136	3,144
Pangani	2,921	3,138	3,151

JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA KWA SHILINGI/LITA

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	2,836.38	2,997.75	2,966.62
Tanga	2,783.47	2,998.81	-
Mtwara	2,882.10	3,043.46	-

Dkt. James A. Mwainyekule
MKURUGENZI MKUU- EWURA